**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**24 Desemba, 2025**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA MCHEZO WA NETIBOLI TANZANIA (CHANETA)

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama na wadau wa mchezo wa Netiboli Tanzania (CHANETA), kuwa uchaguzi wa Viongozi wa Chama hicho unatarajiwa kufanyika tarehe 01 Februari, 2026, Jijini Dodoma.

Fomu za kugombea nafasi tofauti katika uchaguzi huo zitaanza kutolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia tarehe 24 Desemba, 2025 hadi Januari 28, 2026 na zinapatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni www.bmt.go.tz

Aidha, Usaili wa wagombea wa nafasi hizo unatarajiwa kufanyika tarehe 31 Januari, 2026 Jijini Dodoma.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

| Nafasi | Ada |
|---|---|
| 1. Mwenyekiti<br>2. Makamu Mwenyekiti<br>3. Katibu Mkuu<br>4. Katibu Mkuu Msaidizi<br>5. Mweka hazina | 100,000/= |
| 6. Wajumbe (6) | 50,000/= |

**Sifa za wagombea**

- **i.** Awe Raia wa Tanzania
- **ii.** Awe na Elimu isiyopungua Kidato cha Nne (Cheti cha Elimu ya Sekondari)

Uwanja wa Benjamin Mkapa, (Ghorofa ya pili), Barabara ya Taifa, S.L.P 20116, **DAR ES SALAAM.**
**Simu:** +255 (734 220 164 info@nationalsportscouncil.go.tz na **Tovuti**:www.bmt.go.tz

iii. Awe na ujuzi na uzoefu wa uendeshaji wa mchezo wa Netiboli uliothibitishwa wa angalau miaka miwili (2).
iv. Awe anazifahamu Sheria za mchezo wa Netiboli
v. Awe na umri usiopungua miaka ishirini na tano (25)
vi. Awe amewahi kuwa ama mchezaji wa Netiboli, Kocha, Mwamuzi, Kiongozi au kushiriki katika uendeshaji wa mchezo wa Netiboli.

Malipo ya fomu yafanyike katika Akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo ya Serikalini.

Ili kupata namba ya malipo (Control Number) mgombea anashauriwa kupiga namba ya simu ifuatayo; 0683 578 186

Aidha, fomu ya kugombea iwasilishwe Baraza ikiambatishwa na risiti ya malipo pamoja na nakala za nyaraka kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA).

BMT inatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA) kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya Mchezo huo nchini.

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

**BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)**